

HATARI>> Kulaza mtungi kunasababisha gesi iliyopo katika hali ya kimiminika kugusana na valvu

Hatari kwa bodaboda kulaza mitungi ya gesi

Na ZIANA BAKARI

IMEZOELEKA baadhi ya madereva wa pikipiki, bajaji na magari kusafirisha mitungi ya gesi ya kupikia bila kuzingatia usalama.

Idadi kubwa ya madereva hususan bodaboda, husafirisha mitungi ikiwa imelazwa au kuwekwa katika namna ambayo inaweza kusababisha mitungi kusogea, kuanguka au kugongana wakati wa safari.

Kutokuwa na elimu kuhusu madhara ya kubeba mitungi ya gesi ikiwa imelazwa, kumechangia madereva wengi kutochukua tahadhari ya usalama wao na jamii.

Iko hivi. Kubeba au kutumia mitungi wa gesi ya kupikia kuna hatari kubwa, ikiwa msafirishaji au mtumiaji hatachukua tahadhari mapema.

Madhara makubwa yanayoweza kutokea ni pamoja na mlipuko mikubwa inayosababishwa na uvujaji wa gesi, kuanguka kwa moto mkali na kukosa hewa safi kufuatia sumu ya gesi hiyo kuvuja.

Madereva wa bodaboda ndiyo kundi kubwa lililopo hatarini kupata madhara, kwa kuwa mara nyingi wamekuwa wakibeba mitungi ya gesi kwa kuilaza kupeleka kwa wateja.

Akizungumza na gazeti hili hivi karibuni, Konstebo wa jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Misana Mulemwa, alisema miongoni mwa makosa yanayofanywa mara kwa mara ni kusafirisha mitungi ya gesi ikiwa imelala, badala ya kuiweka wima.

Alisema kulaza mitungi kunasababisha gesi iliyopo katika hali ya kimiminika kugusana na valvu, jambo linaloweza kuongeza hatari ya uvujaji endapo valvu itashindwa kufanya kazi ipasavyo.

"Ni makosa kiusalama

kubeba mitungi wa LPG kwa njia ya mlalo, kwa sababu gesi kimiminika inaweza kugusana na valvu, wakati valvu inapaswa kugusana zaidi na gesi iliyopo katika hali ya mvuke.

"Unapolaza mtikisiko unaotokea wakati wa usafirishaji unaweza kuchangia mabadiliko ya shinikizo ndani ya mtungi na kuongeza uwezekano wa gesi kuvuja," alisema.

Alisema kosa jingine linalofanywa na madereva ni kusafirisha bila kufanya ukaguzi wa awali, akieleza ni muhimu kuangalia kama mtungi una mikunjo, umevimba, una mikwaruzo mikubwa au umeathiriwa na kutu.

Mulemwa alisema mitungi yenye dalili hizo haipaswi kuendelea kutumika kwa kuwa inaweza kuwa katika hali isiyofungwa.

Aidha, alisema mitungi inapaswa kusafirishwa katika maeneo yenye uingizaji hewa wa kutosha na aliwataka wasafirishaji kuepuka kuiweka katika buti ya gari au sehemu nyingine iliyofungwa.

"Uingizaji hewa husaidia endapo gesi itavuja isijikusanye na kusababisha mlipuko inapokutana na joto, cheche au chanzo kingine cha moto," alisema Mulemwa.

Mulemwa alisema LPG inayovuja inapochanganyika na hewa katika uwiano wa asilimia 2.1

hadi 9.6 inaweza kusababisha mlipuko mkubwa endapo itakutana na chanzo cha joto, moto au cheche.

Unapolaza mtikisiko unaotokea wakati wa usafirishaji unaweza kuchangia mabadiliko ya shinikizo ndani ya mtungi na kuongeza uwezekano wa gesi kuvuja.

Alisema hali hiyo inaweza kusababisha mlipuko wa wingu la mvuke, maarufu Vapor Cloud Explosion (VCE), endapo gesi hiyo itajikusanya katika kiwango kinachoweza kuwaka ikikutana na chanzo cha kuwasha.

Hatua za kuchukua Akizungumzia hatua za kuchukua wananchi wanapohisi mitungi wa gesi unavuja, waepuke kutumia viberti, sigara au moto wa wazi katika eneo hilo kwa kuwa vinaweza kusababisha cheche na kuwasha gesi iliyovuja.

Alisema wananchi wanapaswa kufunga milango na madirisha kwa tahadhari kuruhusu gesi kutoka nje, kuhakikisha watu wote wanatoka katika eneo hilo kwenda sehemu salama.

Aidha, alitoa wito kwa watumiaji wa nyumbani kuhakikisha mitungi unakuwa wima wakati wote wa matumizi, kuwekwa mbali na vyanzo vya joto au vifaa vinavyoweza kuwaka.

Alisema mitungi unapaswa kuhifadhiwa eneo lenye uingizaji hewa ya kutosha, ikiwezekana nje ya nyumba katika eneo maalumu la kuhifadhi, badala ya kuwekwa ndani ya chumba kisicho na hewa ya kutosha.

Aidha, alisema watumiaji wanapaswa kukagua mara kwa mara bomba la gesi, viungio vya mtungi na jiko kubaini dalili za uvujaji.

"Watumiaji wa nyumbani waache mitungi utulie kwa takribani dakika 30, baada ya kusafirishwa kabla ya kuanza kutumiwa," alisema Mulemwa.

Akirejea miongozo ya usalama ya NFPA 58, Mulemwa alisema, mitungi ya gesi inapaswa kusafirishwa ikiwa imesimama wima na kufungwa vizuri kuzula kusogea, kuanguka au kupata uharibifu wakati wa safari.

"Kifungu cha 9.3.2.8 cha NFPA 58 kinataka mitungi hiyo iwekwe katika hali ya wima, ifungwe kwa usalama wakati wa usafirishaji, lengo ni kupunguza hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na mitungi kuanguka au kugongana," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Ufundi na Mafunzo wa Chama cha Kampuni za Gesi Tanzania (TZLPGA), Huruma Msigwa, alisema miongozo inashauri gesi iwekwe katika 'pallet' kama makasha kuepuka mgongano.

Katika hatua nyingine,



DEREVA wa pikipiki akiwa amebeba mitungi ya gesi kinyume cha utaratibu.



Msimamizi wa Afya na Usalama Mahala pa Kazi, Mazingira na Ujuzi (HSSEQ), Oryx Energies, Ananias Kakwezi, alisema mitungi unapaswa kusafirishwa ukiwa wima.

Alisema mitungi ya gesi isilazwe kwa kuwa Safety Relief Valve (SRV) huwekwa katika sehemu yenye mvuke wa gesi juu ya kimiminika cha LPG.

Alisema mpangilio huo huhakikisha shinikizo ndani ya mitungi linapongezeka na SRV hufunguka, hutoa mvuke wa LPG badala ya kimiminika hivyo kupunguza kiwango cha hatari.

"Kusafirisha mitungi wima ndiyo njia salama inayopendekezwa katika utunzaji na usafirishaji wa mitungi ya

LPG, mitungi uliolazwa unaweza kusababisha ajali," alisema.

Naye, Ofisa Masoko wa Kampuni ya Euro Gas Tanzania iliyopo Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, Juma Mohamed, alisema ni hatari kulaza mitungi wa gesi wakati wa usafirishaji.

Alisema athari ya kulaza mitungi wa gesi valve ikiwa imetumika muda mrefu, inaweza kuvujisha gesi ikaleta madhara kwa kuwa cheche zinaweza kutengeneza mlipuko.

Dereva wa bodaboda, John Peter, akizungumza na gazeti hili alisema idadi kubwa hawana elimu kuhusu namna ya kubeba mitungi wa gesi, hivyo aliomba elimu zaidi itolewe kwa maafisa usafirishaji.

OFISA Ufundi na Mafunzo wa Chama cha Kampuni za Gesi Tanzania (TZLPGA), Huruma Msigwa.